# MKATABA WA KUPANGISHA ENEO KWAAJILI YA MAEGESHO YA MAGARI (YARD)

Kati ya

**PADRE FIDSON MESHACK MWENGO**
**(MWENYE ENEO/MPANGISHAJI)**

Na

1. **ABDI HUSSEIN @ MOHAMED ABDI**
2. **HADIJA YASSIN OSMAN**
3. **AMINA ELIMI AINAN**

**(WAPANGAJI)**

**Umeandaliwa na:**

*Hangi M. Chang'a,*
*Wakili wa Serikali,*
*S.L.P 9050, Dsm,*
*Simu 0784 375 821*
*0767 375 821*
*0715 375 821*

**MKATABA WA KUPANGISHA ENEO KWAAJILI YA MAEGESHO YA MAGARI (YARD)**

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 13 mwezi 02 2016

Kati ya

**PADRE FIDSON MESHACK MWENGO** wa Simu Na. 0718 920 587 na 0755 736 325, Dar es salaam (ambaye katika Mkataba huu ataitwa "**MPANGISHAJI**") kwa upande mmoja;

Na

**ABDI HUSSEIN @ MOHAMED ABDI, HADIJA YASSIN OSMAN** na **AMINA ELIMI AINAN** wa, Dar es salaam (ambao katika Mkataba huu wataitwa "**WAPANGAJI**") kwa upande mwingine.

AMBAPO **MPANGISHAJI** ni mmiliki halali wa eneo lenye ukubwa wa ekari moja lililoko eneo la Buza Wilaya ya Temeke ndani ya Jiji la Dar es salaam.

**MPANGISHAJI** anawapangisha **WAPANGAJI** sehemu hiyo kwa matumizi ya kuegesha magari (yard).

Kwamba kinachopangishwa ni eneo lenye ukubwa wa ekari moja lililoko Buza Wilaya ya Temeke ndani ya Jiji la Dar es salaam.

AMBAPO SASA INAKUBALIWA KUWA:

***Muda wa mkataba na malipo ya pango (eneo)***

1. Mkataba huu ni wa muda wa miaka thelathini (30) kuanzia tarehe 8 Aprili, 2016 hadi tarehe 8 Aprili, 2046. **MPANGISHAJI** amewapa **WAPANGAJI** muda wa kujipanga (grace period) ya miezi miwili yaani kuanzia tarehe 8 Februari, 2016 hadi tarehe 8 Aprili, 2016.

2. Kodi ya yard kwa kila mwezi itaanza kwa kiwango cha **Shilingi za Kitanzania laki saba (T.Shs.700,000/=) tu**

3. Baada ya miaka minne ya kwanza kumalizika, kodi itakuwa inapanda kwa asilimia tatu (3%) kila awamu (msimu) wa kulipa.

4. Kwamba kodi hiyo itakuwa inalipwa kupitia **akaunt namba 23010019978 iliyoko bank ya NMB kwa jina la FIDSON MESHACK MWENGO** ambapo kodi hiyo italipwa kwa awamu kama ifuatavyo;

ATTORNEYS GENERAL'S CHAMBERS 13 FEB 2016 P.O. Box 9050, DAR ES SALAAM

2

kitakuwa na ongezeko la asilimia tatu (3%) ya kodi waliyolipa awamu iliyopita. Malipo hayo yatalipwa miezi miwili kabla ya muda husika kufika.

**KWAMBA PANDE HIZI ZIMEKUBALIANA PIA KAMA IFUATAVYO;**

1. **WAPANGAJI** wameruhusiwa kujenga uzio (ukuta) kuzunguka kiwanja chote na kuacha milango ya kuingilia na kutokea magari. Pia kujenga ofisi itakayotumika kuratibu shughuli za pango hilo.

2. Kwamba ujenzi wa ukuta huo utagharamiwa na **WAPANGAJI**.

3. Kwamba **WAPANGAJI** wanatakiwa kujenga ukuta huo kwa vifaa imara, yaani uwe imara ili kuepusha adhaa zinazoweza kusababishwa na ujenzi usio imara.

4. Kwamba mara baada ya muda wa mkataba kuisha ukuta huo, ofisi na maendelezo yeyote kwenye kiwanja hicho yatabaki kuwa mali ya **MPANGISHAJI**.

5. Kwamba **WAPANGAJI** wataendelea kuyatunza eneo lote walilopanga pasipo kuleta adha kwa majirani.

6. Kwamba **WAPANGAJI** hawaruhusiwi kuegesha magari nje ya eneo walilopangishwa wala kuzuia watumiaji wengine kwa namna moja au nyingine.

7. **WAPANGAJI** hawaruhusiwi kuchukulia mkopo pango hilo au kuweka rehani kwa namna moja au nyingine.

8. **WAPANGAJI** hawaruhusiwi kupangisha eneo hilo kwa mtu mwingine hadi wapate idhini ya maandishi kutoka kwa **MPANGISHAJI.**

9. Kwamba mke wa **MPANGISHAJI** aitwaye **GLLEDA FIDSON MWENGO** naye amekubaliana na kilichojili kwenye mkataba huu na ya kwamba atayaheshimu Masharti haya kama alivyosaini hapa chini.

10. Kwamba, kwa kuwa **WAPANGAJI** wanaruhusiwa kuweka umeme na maji ilimradi wawe wanalipa bili ya umeme na maji kadri wanavyotumia.

11. **MPANGISHAJI** anamhakikishia **WAPANGAJI** kuwa Mkataba huu utadumu kwa muda wote uliokubaliwa isipokuwa endapo masharti ya Mkataba yatakiukwa na **WAPANGAJI**.

ATTORNEYS GENERAL'S CHAMBERS
13 FEB 2018
P.O. Box 9050, DAR ES SALAAM



CamScanner

UMESAINIWA na KUWASILISHWA hapa Dsm na **HADIJA YASSIN OSMAN** ambaye ninamfahamu leo tarehe 13 mwezi Februari, 2016. } ....H. Yassin....

**MPANGAJI**

UMESAINIWA na KUWASILISHWA hapa Dsm na **AMINA ELIMI AINAN** ambaye ninamfahamu leo tarehe 13 mwezi Februari, 2016. } ..........

**MPANGAJI**

MBELE YANGU:

Jina: Hangi M. Chang'a
Saini: ..........
Wadhifa: WAKILI WA SERIKALI

ATTORNEYS GENERAL'S CHAMBERS 13 FEB 2016 P.O. Box 9050, DAR ES SALAAM

MKATABA HUU PIA UMESHUHUDIWA NA:

UPANDE WA **MPANGISHAJI**:

1. Gileda Fidson Mwengo (Mke wa Mpangishaji) Saini: G. F. Mwengo
2. Rev. Fr Yoshua Daudi Mwiguti Saini: ..........

UONGOZI WA SERIKALI ZA MITAA:

Maulid S. Palanga Saini & Mhuri.......... Palanga.

MWENYEKITI WA SERIKALI YA ......
MASHINE YA MAJI

MBELE YANGU:

Jina: Hangi M. Chang'a
Saini: ..........
Wadhifa: WAKILI WA SERIKALI

ATTORNEYS GENERAL'S CHAMBERS 13 FEB 2016 P.O. Box 9050, DAR ES SALAAM



CamScanner

# DIOCESE OF DAR ES SALAAM
## (ANGLICAN CHURCH OF TANZANIA-ACT)


Diocesan Bishop:
[illegible]
[illegible]
[illegible]

Vicar General
[illegible]
Administrative Secretary
[illegible]


Our Ref. No. DD/G5/VI[illegible]/575,

Your Ref. No. PADRE FIDSON MESHACK MWENDO  Date 1/8/2001

**<u>MASHARTI YA KUTUMIA VIWANJA VYA KANISA KWA UJENZI WA NYUMBA YA KUISHI KWA WATUMISHI NA MIZI WA KANISA ANGLIKANA TANZANIA DAYOSISI YA DAR ES SALAAM</u>**

1. Mhusika anaruhusiwa kujenga nyumba ya kudumu sehemu aliyopewa.
2. Nyumba itatumika kwa makazi pamoja na familia yake.
3. Mhusika atawajibika kusaidia ulinzi wa maeneo/viwanja vya Kanisa kutokana na wavamizi.
4. Hakuna ruksa ya kugawa sehemu uliyopewa kwa watu wengine.
5. (a) Endapo mhusika atahama Dayosisi basi nyumba hiyo itauziwa Dayosisi kwa ajili ya watumishi wengine.
   (b) Kama mhusika akifariki dunia, basi mama mjane (mke wake) ataendelea kuishi pamoja na watoto wake.
   (c) Endapo wote watafariki, basi warithi wataiuzia nyumba hiyo kwa Dayosisi (K.A.T.).
6. Hakuna ruksa ya kufanya biashara haramu kama vile pombe pamoja na madawa ya kulevya. Maadili ya Kanisa ni lazima yadumishwe kwenye maeneo yote ya Kanisa.
7. Mhusika atachangia kulipia kodi ya viwanja ya kila mwaka.

- Mimi Revd. Canon/Mwagu/Padre. FIDSON MESHACK MWENGO nimekubali kufuata masharti ya hapo juu.

Sahihi:..(signature)..............

Jina la Mke. Gulela F Mwengo. Sahihi....G. Mwengo........

Jina la Shahidi Rev. FR. PAUL C. [illegible] Sahihi....(signature)........

Katibu..REV. FR NOEL MAMBO.............. Sahihi....................

Muhuri wa ofisi
VICAR GENERAL....ACT DIOCESE OF DAR ES SALAAM....

Msajili wa Dayosisi..(signature)..............

Askofu wa Dayosisi..(signature)..........

Tarehe....1.-.8.-..... 19.2001....

ANGLICAN CHURCH OF TANZANIA (A.C.T.)
DIOCESE OF DAR ES SALAAM
P.O. Box 25016
DAR-ES-SALAAM

12. **WAPANGAJI** wanamhakikishia **MPANGISHAJI** kuwa watamkabidhi pango hilo bila masharti yoyote mara Mkataba utakapoisha na ikiwa watahitaji kuendelea na upangaji wa sehemu hiyo watalazimika kutoa taarifa ndani ya miezi mitano (5) kabla ya muda wa Mkataba kuisha, ambapo **MPANGISHAJI** ataamua kuendelea au kutoaendelea kumpangishia **WAPANGAJI**.

13. **WAPANGAJI** anatakiwa kuweka mazingira safi na pia hapaswi kubadilisha matumizi aliyoombea sehemu hiyo bila idhini ya **MPANGISHAJI**.

14. Kwamba likitokea jambo lolote la kuweza kuzuia kuendelea kwa mkataba huu ambalo halijasababishwa na upande wowote, itabidi **MPANGISHAJI** awarudishie hela ya miezi ambayo watakuwa hawajatumia pango hilo.

15. Kwamba mkataba huu utawabana pia ndugu, warithi, jamaa wa pande zote mbili katika mkataba huu.

16. Kwamba, endapo patatokea kutoelewana baada ya kusaini Mkataba huu, basi upande utakaoathirika uwasiliane na mwandishi wa mkataba huu au **WAKILI** yeyote anayekubalika na pande zote ili aangalie uwezekano wa kusuluhisha mgogoro huo kabla ya kuchukua hatua zingine kisheria dhidi ya upande mwingine.

KWA KUSHUHUDIA pande zote mbili zinaweka saini zao leo tarehe, mwezi na mwaka kama inavyoonekana hapa chini:



UMESAINIWA na KUWASILISHWA hapa Dar es salaam na **PADRE FIDSON MESHAKI MWENGO** ambaye ninamfahamu leo tarehe 13 mwezi Februari, 2016.

........................ **MPANGISHAJI**

MBELE YANGU:

Jina: Hangi M. Changa

Saini: ........................

Wadhifa: WAKILI WA SERIKALI

13 FEB 2016

UMESAINIWA na KUWASILISHWA hapa Dsm na **ABDI HUSSEIN @ MOHAMED ABDI** ambaye ninamfahamu leo tarehe 13 mwezi Februari, 2016.

**MPANGAJI**

13 FEB 2016

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

KATA YA BUZA
OFISI YA SERIKALI YA MTAA
MASHINE YA MAJI,
DAR ES SALAAM

Tarehe 08/02/2016

S. L. P 46343,
SIM: 0784434463
KUMB.TMC/BUZ/MMJ/ G50/02/2016
KWA: ABDI HAKIMU ZHADIA JASH
IBDILLAHI ELMI AINANA
MOHAMED ABDI



YAH: UTAMBULISHO WA MKAZI.

---

Tafadhari rejea kichwa cha habari hapo juu.

Nathibitisha kuwa bw/bi EDISON MESHACK MUTINGO Ambaye picha yake ipo hapo juu kuwa ni mkazi halali wa mtaa huu

Kazi yake ni MCHUNGAJI Amezaliwa tarehe 1966 kijiji/mtaa/wilaya KASULU Mkoa KIGOMA Namba yake ya simu 0755736325

Anaishi Nyumba No.mm/ DD165/KIWANGA/373 Ninakili kumtambua baada ya kutambulishwa kwangu na mjumbe wake wa shina No. 30 Wa eneo lake Ndugu ALFONS BONAVA Ambaye amenithibitishia kumtambua.

Anashida yake ya NI MMILIKI WA KIWANJA CHENYE NAMBA TAJWA HAPO JUU. KILICHOPO CHAMBA LA KANISA ANGLICANA BUZA

Ofisi yangu hii haina pingamizi lolote naomba asaidiwe kwa mujibu wa taratibu za ofisi yako.

WAKO KATIKA KAZI

MAULID. S. PALANGA

MWENYEKITI WA SERIKALI YA MTAA.

CamScanner

i) Awamu ya kwanza itakuwa ni ya malipo ya kipindi cha miaka minne yaani kuanzia tarehe 8 Aprili, 2016 hadi tarehe 8 Aprili, 2020 ambapo **WAPANGAJI** watalipa kwa awamu mbili. Mara ya kwanza watalipa kodi ya miaka miwili kiasi cha **Shilingi za Kitanzania milioni kumi na sita na laki nane (T.Shs.16,800,000/=) tu**. Mara ya pili **WAPANGAJI** watamalizia kulipa kodi ya pango ya muda wa miaka miwili iliyosalia kukamilisha miaka minne ya awamu ya kwanza kiasi cha **Shilingi za Kitanzania milioni kumi na sita na laki nane (T.Shs.16,800,000/=) tu.** Kodi hiyo italipwa tarehe 1 Agost, 2016.

ii) Awamu ya pili itakuwa ni ya malipo ya kipindi cha miaka mitano yaani kuanzia tarehe 9 Aprili, 2020 hadi tarehe 9 Aprili, 2025 ambapo **WAPANGAJI** watalipa kwa mkupuo. Kiasi cha kodi watakacholipa kitakuwa na ongezeko la asilimia tatu (3%) ya kodi ya sasa. Malipo hayo yatalipwa miezi miwili kabla ya muda husika kufika.

iii) Awamu ya tatu itakuwa ni ya malipo ya kipindi cha miaka mitano yaani kuanzia tarehe 9 Aprili, 2026 hadi tarehe 9 Aprili, 2030 ambapo **WAPANGAJI** watalipa kwa mkupuo. Kiasi cha kodi watakacholipa kitakuwa na ongezeko la asilimia tatu (3%) ya kodi waliyolipa awamu iliyopita. Malipo hayo yatalipwa miezi miwili kabla ya muda husika kufika.

iv) Awamu ya nne itakuwa ni ya malipo ya kipindi cha miaka mitano yaani kuanzia tarehe 9 Aprili, 2030 hadi tarehe 9 Aprili, 2035 ambapo **WAPANGAJI** watalipa kwa mkupuo. Kiasi cha kodi watakacholipa kitakuwa na ongezeko la asilimia tatu (3%) ya kodi waliyolipa awamu iliyopita. Malipo hayo yatalipwa miezi miwili kabla ya muda husika kufika.

v) Awamu ya tano itakuwa ni ya malipo ya kipindi cha miaka mitano yaani kuanzia tarehe 9 Aprili, 2035 hadi tarehe 9 Aprili, 2040 ambapo **WAPANGAJI** watalipa kwa mkupuo. Kiasi cha kodi watakacholipa kitakuwa na ongezeko la asilimia tatu (3%) ya kodi waliyolipa awamu iliyopita. Malipo hayo yatalipwa miezi miwili kabla ya muda husika kufika.

vi) Awamu ya sita na ya mwisho itakuwa ni ya malipo ya kipindi cha miaka sita yaani kuanzia tarehe 9 Aprili, 2040 hadi tarehe 9 Aprili, 2046 ambapo **WAPANGAJI** watalipa kwa mkupuo. Kiasi cha kodi watakacholipa

ATTORNEY'S GENERAL'S CHAMBERS
13 FEB 2016
P.O. Box 9050, DAR ES SALAAM